JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAMISEMI.

Shule ya Sekondari Kizwite,
S.L.P. 215,
SUMBAWANGA

Kumb.Na: ……

Tarehe……/……/20…….

Jina la Mwanafunzi……
……..
S.L.P……..

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIZWITE

1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kidato cha **Kwanza** katika shule hii mwaka **2021.**Shule ya Sekondari Kizwite ipo Kata ya Kizwite Manispaa ya Sumbawanga.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **11.01.2021.** Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11.01.2021** hivyo ndani ya siku saba (7) unatakiwa uwe umeripoti,vinginevyo nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi wa akiba.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A. SARE YA SHULE:

i) WAVULANA:

Suruali: Anatakiwa awe na suruali mbili nyeusi na Khaki (Rangi ya Vitambaa imeambatanishwa). Mshono wa Suruali: iwe na mifuko mitatu mmoja nyuma upande wa kulia na miwili pande zote kulia na kushoto pembeni **na siyo ya kubandika** ,iwe na rinda mbili kila upande upindo wa chini(miguuni) ugeuzwe juu (turn up) upana miguuni uwe wa kutosha isiwe ya kubana.Suruali za mitumba na jeans haziruhusiwi hapa shuleni.

Shati: Awe na mashati mawili meupe (White) yenye mikono mifupi (Short sleeves)

Viatu: Awe na viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kamba na soksi rangi nyeusi, visiwe na sori ndefu na visivyochongoka mbele.

Sweta: Rangi ya zambarau yenye shingo "V" kwa ajili ya kujikinga na baridi.

Sare ya Michezo: Awe na Physical Training short (P.T. Short) au Tracksuit rangi ya Blue bahari na raba kwa ajili ya Michezo.

Nywele: Nywele ziwe fupi muda wote

ii) WASICHANA:

Sketi: Anatakiwa awe na sketi mbili (2) Nyeusi na Khaki (Rangi ya Vitambaa imeambatanishwa) Mshono wa sketi; Ziwe na marinda kumi na mbili (12). **NB**: Sketi ziwe ndefu zifike kwenye **viatu** , sketi fupi hazihitajiki .Hivyo mzazi unatakiwa kumshonea sketi ndefu ili kuondoa usumbufu unaoweza kujitokeza.

Shati: Awe na mashati mawili meupe (White) yenye mikono mifupi (Short sleeves)

Viatu: Awe na viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kamba na soksi rangi nyeupe, visiwe na sori ndefu na visivyochongoka mbele.

Sweta : Rangi ya zambarau yenye shingo "V" kwa ajili ya kujikinga na baridi.

Sare ya Michezo: Awe na Tracksuit rangi ya Blue bahari na raba kwa ajili ya Michezo.

Nywele: Nywele ziwe fupi muda wote, hakuna kusuka nywele pia kuweka dawa**.**

NB:*Mzazi ambaye atashindwa kuzingatia maelekezo ya ushonaji wa uniform (sale) hatasajiliwa hadi akamilishe maelekezo ya mishono ya uniform (Sale) hasa sketi na suruali.*

2.1 VIFAA VYA MASOMO:

1. Daftari kubwa zisizopungua 12 (Counter Book)
2. Mathematical Set (Mkebe) 1
3. Aje na Kamusi ya Kiingereza (Dictionary) moja.
4. Aje na kalamu za kutosha, rula na penseli.

3.0 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu **Na.25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria **Na.10** ya mwaka **1995**.Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
i) Kutunza mali ya umma.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro.
iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv) Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzake, mwalimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v) Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
vi) Kusuka mwenye kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii) Kufuga ndevu.
viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix) Uvutaji wa sigara.
x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi) Kudharau bendera ya Taifa.
xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

NB:

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Nakutakia maandalizi mema na,

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIZWITE
SUMBAWANGA

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIZWITE

A: MWANAFUNZI

1. Mimi……..Mvulana/Msichana,nimekubali/sikubali kujiunga na shule ya sekondari Kizwite kama mwanafunzi wa kutwa tarehe…….. Wakati wote nitakapokuwa hapa, naahidi kuwa mtiifu, kufuata sheria na kuzingatia taratibu za shule, kama kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai, kutunza mali ya umma na kufanya kazi kadiri ya uwezo wangu. Pia nitakuwa mwanafunzi mwenye Bidii katika masomo na kazi zote za nje(kujitegemea) na nitafika shuleni kila siku bila kuchelewa

2. Nafahamu kwamba kitendo chochote kilicho kinyume na mwenendo na taratibu za shule kinastahili adhabu kali hata kufukuzwa shule kama itakavyoamuriwa na jumuiya pamoja na baraza la ushauri la shule.

3. Sahihi ya Mwanafunzi…….. Tarehe……..

B: SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

1. Mimi……..mzazi/mlezi nimekubali/sikubali mtoto wangu(Jina)…….asome katika shule ya sekondari Kizwite kuanzia tarehe……..
2. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote anayotakiwa kuwa nayo shuleni kama ilivyotajwa katika barua hii.
3. Ninakuhakikishia kwamba nitamuonya mtoto wangu kutii sheria na taratibu zote za shule na kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai pia kuishi maisha yenye mwelekeo na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea.
4. Ninaahidi kuwa mtoto wangu atafanya kazi zote za Elimu ya Kujitegemea(E.K) kwa mikono yake kwa juhudi na maarifa bila kushurutishwa.

Jina la Mzazi/Mlezi:……

Sahihi ya Mzazi/Mlezi:……..

Anuani ya Mzazi/Mlezi:……

Namba za simu za Mzazi/ Mlezi:……..

Tarehe……

NB:*Jaza hii fomu na urudishe shuleni*.

HISTORIA YA MWANAFUNZI NA TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI .

1. Jina kamili la mwanafunzi……Kabila……Dini……
2. Tarehe ya kuzaliwa……..Mahali alipozaliwa……Uraia……
3. Shule alipo maliza darasa la saba……..
4. Jina la Baba :……Hai/Amefariki……..
5. Jina la Mama…… Hai/Amefariki……..
6. Jina kamili la Mlezi(kama hana wazazi)……..
7. Uhusiano na Mlezi……..
8. Kazi ya Baba /Mlezi……..
    - Anuani yake……
    - Namba ya simu……kwaajili ya mawasiliano .
9. Mtaa/kitongoji/eneo analo ishi……
10. Jina la mwenyekiti wa mtaa……..Namba yake ya simu……
11. Shule ya Msingi anayotoka mwanafunzi……..
12. Jamaa /Ndugu wengine anaowategemea :
    a) ……..uhusiano wake……
    b) ……..uhusiano wake……
    c) ……..uhusiano wake……
    d) ……..uhusiano wake……
    e) ……..uhusiano wake……
13. Ujuzi (Stadi) mwingine alionao mwanafunzi……

    ……..

NB:*Jaza hii fomu na urudishe shuleni.*

KIZWITE SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 215,
SUMBAWANGA – RUKWA

MEDICAL OFFICER,
……..
……..
……..

RE: MEDICAL EXAMINATION:

MR/MISS: ……..

Please examine the above named pupil as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this School. The examination should include the following categories.

1. Hemoglobin ……..
2. P.V. Bleeding ……..
3. Sight ……..
4. Blood pressure ……..
5. Urine for Sugar and Pregnancy……
6. Stool for routine examination ……..
7. Asthma ……..
8. Skin/Diseases ……..
9. Leprosy ……..
10. Pulmonary tuberculosis……..
11. Neurosis ……..
12. Venereal diseases ……..
13. Other serious diseases ……..

PART B:

MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by a Government Medical Officer)

1. I have examined the above named pupil and Consider that he/she is Physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full schooling.
2. Other comments: ……
   ……..

DATE:…… ……

SIGNATURE AND OFFICIAL STAMP

NB:*Nenda hospitali na fomuhii kwaajili ya vipimo,kisha irudishe shuleni*.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ,
Wilaya yaSumbawanga
S.L.P 116
SUMBAWANGA.

Tarehe……..

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Kizwite
S.L.P 215
SUMBAWANGA.

UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA.

Nathibitisha kuwa……..(Jina kamili la mwanafunzi) ni Raia wa Tanzania kwa Kuzaliwa/Kuandikishwa.

Baba yake (Jina kamili)……..amezaliwa katika Mkoa wa ……..Kata ya……..Tarafa ya ……Wilaya ya……..hapa Nchini.

Mama yake (Jina kamili) ……..amezaliwa katika Mkoa wa ……..Kata ya……..Tarafa ya ……Wilaya ya……..hapa Nchini.

……
MKUU WA WILAYA

NB:*Kila mwanafunzi analazimika kuishughulikia Fomu hii kikamilifu.Ikijazwa irudishwe kwa Mkuu wa Shule tarehe ya kuripoti Shuleni. Kama ana cheti cha kuzaliwa aje na Nakala (Fomu hii asijaze).*